# *Yehova-Yire*

. . .sana Ndugu Buntain.

2 Habari za asubuhi kwa darasa, ni ma—majaliwa kuwa hapa. Jana ilikuwa siku ya mwanga mwekundu katika, ama, siku ya kumbukumbu, nilipaswa kusema, katika huduma yangu. Nafikiri ndugu aliyetafsiri hiki anataka kuja kukisoma mwenyewe moja ya siku hizi juu ya yale yaliyosemwa jana, na jambo la ajabu sana likatukia.

3 Nami nina kijitabu ambacho mtu fulani amekisambaza hapa, kinachoitwa *Mwandishi Mbaptisti*, Nafikiri ilikuwa ni Ndugu Paul Boyd, nina hakika kabisa. Someni hicho, kama ana vingine. Hicho, kamwe sikukisoma mpaka asubuhi ya leo, nijuavyo mimi.

4 Nami ni—nilikuwa nikikisoma, niliamka tu mapema, nami ninapenda kuamka mapema Jumapili asubuhi na kutembea-tembea, mwajua, karibu ma—makazi yote ya pepo huwa nje usiku sana, wamelala, ndipo basi unaweza kutoka nje kwenye baridi na upendo wa asubuhi. Ni kama tu, vema, mwajua, mazingira ya usiku yanavyoshuka, unaweza kutoka nje, unaweza kunusa harufu ya—ya mchongomvu, na maua, na kadhalika, kwa sababu ni utamu wa asubuhi ndio unaoleta umande huo na unabeba harufu nzuri.

5 Na hivyo ndivyo ninavyodhania inatupasa kufanya sikuzote tunapokuja kwenye mimbara yetu, ni kujifungia ndani pamoja na Mungu, huku ulimwengu ukiwa nje, ili uweze kutembea pamoja na—kwa upako wa Roho Mtakatifu. Mzuri sana! Naupenda sana.

6 Nilikuwa nimesimama huko nyuma dakika chache zilizopita, ndipo nikasikia wimbo huo ukianza, *Amini Tu*, nikamwangalia mwanangu na Ndugu Borders, nami nikasema, "Wazieni tu, wimbo hu—huo umenialika jukwaani katika, nadhani, lugha arobaini mbalimbali, kote ulimwenguni."

7 Ninakumbuka, nilikuwa nimeketi miguuni pa Paul Rader wakati alipouandika huo. Ni wangapi waliopata kusikia habari za Paul Rader? Hakika, karibu sote tulizisikia, kule, ndugu Mbaptisti kwenye Maskani ya Injili ya Fort Wayne. Nami ninakumbuka jinsi ulivyosikika mtamu sana kwangu, daima unasikika mtamu, bali umekuwa ndio wimbo wangu mrejeo, sasa, kwa miaka kumi na minne, tangu nimekuwa hudumani.

8 Nami nakumbuka nikiketi huko nyuma kwenye Maskani ya Rediger pale nilipokuwa. . .Maskani ya Injili ya Fort Wayne nilipokuwa na ibada, nami nilikuwa nimeketi kwenye chumba cha kusomea cha Paul, papo hapo alipoandika wimbo huo,

nami nilikuwa nimeketi pale, nilikuwa nikizungumza na F. F. Bosworth, na—na wahudumu fulani, kabla tu ya kwenda mimbarani, ndipo kwa utamu ukawa unavumia kwenye spika hiyo, loo, jamani, nikawaza, "Paul, laiti ningaliweza kukupa mkono sasa," mwajua. Mnajua, alikuwa, Paul alikuwa mtu mashuhuri wa Mungu, kweli alikuwa, hodari wa kuwaleta watu wengi.

9 Mwajua, maneno yake ya mwisho huku juu, wakati alipokuwa akifa, alikuta makaburi hapa, na hilo likamwua. Kwa hiyo, alipokuwa akifa, alisema—alisema, "Kama mimi," alipoweka mkono wake juu ya bega la ndu—ndugu mmoja, ilikuwa ni rafiki yangu, angali hai leo, akasema, "kama ningaliuza ujumbe wangu wa neema kwa hao Wapentekoste motomoto sana, badala ya kuwatupia ninyi Wabaptisti, ningekuwa . . . ningekuwa na maisha marefu zaidi."

10 Na hiyo ni kweli. Kasema ujumbe wake wa neema kwa Wapentekoste, badala ya ku—kusumbuka tu na kubanwa kabisa, na *hili*, na lile hekalu kubwa, na mradi wa ujenzi, alikuwa ni mtu wa kiroho, kwa hiyo iliusonga tu uhai ukamtoka, na kumpa kansa, ndipo akafa.

11 Kabla tu hajafa, alimwita ndugu yake, Luke. Moody Bible, huko Chicago, ilikuwa imetuma maskini wa—waimbaji wanne wamwimbie. Naye Paul daima alikuwa mcheshi. Nadhani mlimjua Paul, jinsi . . .

12 Naye Luke alimzidi ucheshi, Luke alikuwa mwana mizaha mkubwa, usingeweza kujua ni wakati gani alikuwa anasema kweli. Alizoea kuingia mkahawani, nao walikuwa, walipokuwa na hii . . . Ni kitu gani, Gene, mnakiitaje kitu hiki mlichokuwa nacho, kwa namna fulani kirefu . . .? Mwajua, kimezungushwa, kimezungushwa, wanacho katika vipande vidogo sasa. Namna fulani—namna fulani . . . La, ni—ni nafaka ya kiamshakinywa. Ngano Zilizopasuliwa. Alikuwa na vitu hivyo vidogo, virefu namna hiyo, naye aliviita *magodoro ya wanasesere*. Akamwambia huyo mama, "Niletee magodoro ya wanasesere." Alikuwa mlafi kupindukia.

Ndipo akamwambia yule mama asubuhi moja:

Kasema, "Utakula nini?" Msichana mdogo wa kusini.

Akasema, "Vema, nitakula nusu dazani ya mayai, na ratili moja ya hemu, na takriban biskuti kumi."

Akatikisatikisa maskini mguu wake, akasema, "Sasa utakapoamua kuniambia unachotaka!"

Akasema, "Hicho ndicho ninachotaka," naye alikuwa mlafi hodari.

"Hicho," Ndugu Bosworth akasema, "hicho ndicho anachotaka."

Akasema, “Kwani kuna nini? Hivi hamjazoea kuwalisha wanaume huku chini kusini?”

Msichana huyo akasema, “Naam, bwana, lakini sio kujaza maghala.” A—alikuwa na ucheshi sana.

13 Paul, alipokuwa akifa, na hapa juu hospitalini, Los Angeles, na wakati yeye—yeye aliposema. . .Paul na ndugu yake walishikana, waliambatana kama mimi na Billy, wakienda pamoja, daima walishikana. Na kwa hiyo, a—akasema, “Yu wapi Luke?” Naye Luke hakumtaka, kumwona akifa, alikuwa ameingia chumba kingine.

14 Hiyo, na maskini hiyo kwaya ilikuwa ikiimba, ama, maskini hilo kundi la waimbaji wanne likiimba *Karibu Zaidi Na Wewe, Mungu Wangu*, Paul kwa namna fulani akajirudia, akaangalia kote, akasema, “Kwani ni nani anayekufa, mimi au ninyi?” Muziki huo wote wa maombolezo. Akasema, “Fungueni hizo pazia, na mniimbie nyimbo motomoto za Injili.”

Kwa hiyo wakaanza kuimba, “Pale msalabani ambapo Mwokozi wangu alifia.”

Kasema, “Huo unasikika bora zaidi.” Kasema, “Yuko wapi Luke?”

Wakasema, “Yuko huko nje kwenye chumba kingine.”

15 Kasema, “Mwambieni aje hapa.” Luke akaingia, kwa namna fulani akijizuiazuia pumzi, alijua ndugu yake alikuwa yuafa, kwa hiyo alisema alinyosha mkono, na kuushika mkono wake, na kusema, “Luke, tumetoka mbali pamoja, sivyo?”

Kasema, “Naam, ndivyo, Paul.”

16 Kasema, “Wazia hilo, katika dakika tano tangu sasa, nitakuwa nimesimama katika Uwepo wa Yesu Kristo, nimevikwa haki Yake,” akauminya mkono wa ndugu yake, akafa. Loo, hiyo ndiyo njia! Jambo ndilo hilo.

17 Nilisimama pamoja na Dk. Bosworth alipoondoka; kisha nikasikia ushuhuda wa Moody alipoondoka; nasi hatuna budi kuondoka, pia. Nimewashika mikononi mwangu, na kuwahisi wakifa, wakiingia baridi, kisha wanajinyosha tena, wakilia wapate rehema na kuomba msaada; nimewaona wakisema, “Nilaze kifuani mwako, Ndugu Branham,” wakainua mikono yao na kuimba:

> Ni siku ya furaha, siku ya furaha,
> Tangu Yesu alipoosha dhambi zangu!
> Alinifundisha jinsi ya kukesha na kuomba.

18 Ninamkumbuka maskini rafiki yangu, nilikuwa nimemshika, akasema, “Hivi huwezi kumwona, Ndugu Branham? Huyo hapo anakuja.” Akasema, “Vema, kwaheri, Ndugu, hata itakapokufikisha kwenye Ufuko wa pili.” Akainua mikono yake, akasema, “Nitakuona kwenye Pwani ya pili.”

Akasema, "Loo, Bwana Yesu!" Naye akainamisha kichwa chake na kuanguka pajani mwangu. Mnaona? Hiyo ndiyo njia ya kwenda, mnaona, hiyo ni kweli. Alikuwa ni mvulana mpendwa, mtakatifu.

19 Nalo, ninaamini kuna wakati mmoja ilipoandikwa katika Maandiko, kwamba Daudi, ninaamini, alisema alikuwa amewaona wasio haki mamlakani, huku wakienea kama mwerezi mbichi, wakifanikiwa tu, na kufanya kila kitu, bali Bwana alimwambia Daudi, "Lakini uliwahi kumwona mwishoni?" Hapo ndipo panapojalisha, si yale yaliyoko hapa, ni yale, ya mwishoni. Na hiyo ndiyo sababu ninajaribu kwa moyo wangu wote, kuwaacha . . . kuwaelekeza watu hadi mwisho.

20 Sasa, kabla sijamaliza ujumbe huu asubuhi ya leo, Bwana akipenda, lakini hii ndiyo sababu inanibidi kusisitiza jambo hilo, endapo hamwezi kulishika kiroho . . .

21 Aisee, wewe uliyeniandikia barua, huko nje kuhusu Ezekieli 33:33, umegonga penyewe, lakini tulia.

22 Sasa, wakati—wakati akienda . . . Ern Baxter aliniambia, alisema kwamba huko Canada walikuwa na ma—mashindano ya kushindania baiskeli hii mpya ya Schwinn, walikuwa wakitaka kufanya shindano la ni nani angeweza kuendesha, naamini, yadi mia moja kwenye ubao, inchi kumi na nne ama kumi na sita mraba, bila kuanguka kutoka kwenye hanamu ya futi mbili, futi tatu, ashuke moja kwa moja kwenye hanamu hiyo, yule ambaye angeweza kuendesha karibu sana na mwisho, huyo ndiye angetunukiwa hiyo baiskeli.

23 Vema, Ern alisema alijua alikuwa anaenda kuishinda, akasema kwa sababu angeweza kwenda katikati ya mji, amnunulie mama yake vyakula, na hata asiguse usukani, kasema kashuka tu chini, unajua jinsi unavyoendesha baiskeli, kasema walikuwa tu ni waendeshaji hodari.

24 Kasema wakati wote walipofika kule siku hiyo kuiendesha, alisema walikuwa na maskini mvulana dondoadume, alionekana kama jamaa mdogo, mnyonge, naye ndiye pekee aliyeiendesha. Aliiendesha moja kwa moja, moja kwa moja mpaka mwisho, akashuka kwenye baiskeli yake, kila mmoja wao alianguka kabla kamwe hawajaenda umbali wowote. Kwa hiyo wote wakazunguka, hao wavulana wakamzunguka, na kusema, "Ulifanikiwaje? Ulilifanyaje?"

25 Akasema, "Sasa, enyi jamaa, nitawaambia i—ilikuwa ni nini." Akasema, "Niliona kila mmoja wenu, mahali mlipokosea," kisha kasema, "nikafanikiwa kwa kosa lenu." Kasema, "Ulipopanda baiskeli yako, nao wakakusukuma uende," kasema, "Niliwaona *hivi*, mkijaribu kuiweka kwenye ubao." Akasema, "Mnaona, unapoangalia chini namna *hii*, unashikwa na wasiwasi." Akasema, "Waliponisukuma, nilielekeza jicho langu kwenye mwisho, na kushikilia imara."

26 Haya basi. Unaona, jambo ndilo hilo, rafiki, usiangalie hapa chini yale yanayoendelea leo au kesho, angalia mwisho, na uwe thabiti. Unaona? Kama utaangalia, na, "Vema, nisipofanya *hili*, nisipofanya *hili*, kama nikininii…" unaona, bila shaka utaanguka, unaona. Angalia mwisho, na mwishoni mwa kila maisha utakutana na Yesu. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo angalia tu mwisho, na uwe imara.

Na tuombe.

27 Baba Mungu, tunaingia sasa Mbele Zako, katika mahali Pako patakatifu, ambapo wema wa Mungu umewekwa kwa ajili ya hao, ile Mana iliyofichwa. Ninaomba Mungu, ya kwamba utatuelezea wazi asubuhi ya leo, katika dakika hizi chache za somo, kumalizia somo hili kuu juu ya mtumishi Wako, yule mzee wetu mkuu Ibrahimu.

28 Tunakushukuru kwa ajili ya kanisa hili na kwa ajili ya milango yake iliyofunguliwa, tunakushukuru kwa ajili ya mchungaji na msimamo wake hodari. Na kumwona, Baba, jinsi anavyobarikiwa na kusaidiwa, tuna furaha sana kwa ajili ya jambo hilo. Ninawazia juu ya maskini yule baba yake mpendwa huko Canada, na jinsi ambavyo alitetea yale yaliyokuwa sahihi katika siku zake, saa zake. Mungu, jalia mwanawe afuate nyayo hizo wala asipatane kamwe, bali adumu moja kwa moja na Roho na Injili. Ninaliombea kanisa lake hapa, watu hawa wa kupendeza ambao wameitwa waingie.

29 Baba wa Mbinguni, unatuleta kwenye nyumba ya masahihisho, nayo masahihisho huanzia katika nyumba ya Mungu, hukumu huanzia hapa. Na kama sisi…Dhambi za baadhi ya watu huwatangulia, wengine zinawafuata, Bwana, jalia zetu zitutangulie tunapokiri kwamba tumekosea, na jalia tupate rehema na neema kutoka kwa Mwanao, Yesu.

30 Wabariki wageni wote malangoni petu, tunaomba ya kwamba utawapa Roho Wako kwa wingi sana. Na jalia uamsho huu mdogo ulioanza sasa, kamwe usiishe mpaka Yesu atakapokuja, tujalie, jalia kuwe na moto mdogo mioyoni mwetu sote.

31 Nami nina hakika, Bwana, ya kwamba wote wanaelewa m—msimamo ninaochukua kwa ajili Yako, kwamba hauna budi kuwa mnyofu, ni njia nyembamba, wala hakuna nafasi barabarani, bali kwa huyo mtu mmoja tu na Yesu pekee, kwa hiyo ni, hatuna budi kutembea hivyo, Bwana. Ninaomba ya kwamba hili kusanyiko litashika ono hilo, na jalia lisiondoke mioyoni mwao, lijalie.

32 Tubariki usiku kucha, tunapokuja kwenye ibada za uponyaji usiku wa leo, jalia kuwe na ibada yenye nguvu sana ya nguvu Zako za uponyaji, usiku wa leo, kuwafanya viwete watembee, vipofu waone. Jalia waingie, Bwana, na kujifungia ndani pamoja Nawe, na kukuangalia Wewe. Roho Wako mkuu na awe hapa.

Jalia wasije na udanganyifu wowote, wala kuja kwa njia yoyote, bali chini tu ya matarajio makuu, kwamba utawamwagia baraka Zako nyingi na kuwapa shauku ya moyo wao, kwa kuwa tunaamini ni mapenzi ya Baba kuwa mwema kwa watoto Wake wote.

33 Imeandikwa katika Maandiko, "Juu ya yote nataka mfanikiwe katika afya." Kwa kuwa Bwana, hatuwezi kukutumikia wakati tunapojisikia wagonjwa, na kudhoofika, bali tunapojisikia vizuri sana, ndipo tunapoweza kufanya vizuri tuwezavyo, nami naomba ya kwamba utatusaidia kufanya vizuri kabisa, kupitia Jina la Yesu Kristo. Amina.

34 Sasa, usiku wa leo, ningetaka kuwafanya watu wote . . . Sasa, kutakuwa na muda kidogo tu wa kusambaza kadi za maombi, hao wavulana watakuwa hapa kusambaza kadi za maombi, basi saa kumi na mbili wawe wameketi papa hapa katika viti *hivi*, moja kwa moja *hapa* ndani. Ndipo watakuja hapa mbele zenu, wachanganye hizo kadi, wawapeni. Sasa, hakikisheni, saa kumi na mbili.

35 Sasa, usipokuja, basi huwezi . . . Na hebu mtu huyo aje, sasa, wale ambao wamekuwa wakipata maagizo ya mikutano, hizo kadi hazibadilishwi, msizitoe na kuwapa akina Jones, naye kamwe hatakuja, na kama hapo, wewe chukua kadi yako na kuketi chini, ungoje tu hapo mpaka wakati wa kuitwa utakapofika.

36 Kisha uwe hapa saa kumi na mbili kamili, maana nafikiri wana mazoezi mengine hapa ya, nijuavyo mimi karibu makanisa yote yafanyavyo, kama hayo yote, kwa hiyo wao, tunawatakeni mje hapa mapema ili tuweze kuliondoa hili mikononi mwetu, ndipo basi nitakuwa nimemaliza basi yapata saa moja na nusu, saa mbili kasorobo, kitu kama hicho nafikiri ndivyo (Sivyo, Ndugu?), kuwaombea wagonjwa.

37 Na sasa, ningetaka kwamba daima mngewaachia wagonjwa viti hivi vya mbele, kama ninaweza kuwaleta hapa juu, mnaona, niwaweke moja kwa moja karibu nami. Jana usiku ilinibidi kutembea kidogo baadaye, upako ulishuka baada ya mimi, nikininii tu, kuuchambua ujumbe huo kwa nguvu sana, mnaona, Roho wa Bwana, ndipo akashuka chini kutoa, kutoa upambanuzi, na kadhalika. Basi kulikuwa na mtu aliyeketi nyuma yangu hapa, ndugu mpendwa, niligeuka na kuona kitu fulani, nikamwashiria kwa kichwa changu, nami nikakutana naye huko nje chumbani, basi ninatumaini kwa Mungu yote yamekwisha sasa. Na kwa hiyo, inaninii tu, inakubidi kuwa mwangalifu.

38 Watu wanafikiri hili ni rahisi sana, hili ndilo jambo gumu sana ulilowahi kuingia. Nimesema mambo, kisha ninaenda nyumbani na kulia mpaka foronya yangu ingelowa. Nimemfanya mke wangu, aje akanikumbatie, nikaketi katikati ya sakafu

nikilia, usiku. I—inakubidi kufanya mambo usiyotaka kufanya, unaona, huyo ni Roho anayefanya hivyo. Hu—huwezi kuwa chochote ila kile ulicho hasa. Unaona? Una. . .Kama hutafuata mwongozo wa roho ya—yako, basi ukifanya jambo ambalo hujisikii kuongozwa kufanya, basi—basi unakuwa mnafiki, unaona. Kuwa kile ulicho, haijalishi wewe ni nini, kuwa hivyo, unaona, kuwa tu hivyo. Basi inaifanya kuwa ngumu sana.

39 Halafu wakati mwingine wakati upako unaposhuka, nawe unaweza kuangalia huko na kuona mambo. Hapa hivi majuzi nilikuwa nimeketi mezani pamoja na—pamoja na baadhi ya wahudumu. Loo, laiti nisingaliketi chini pale. Ndio kwanza—ndio kwanza nitoke tu mkutanoni, walitaka niende kula chakula cha jioni pamoja nao, na hapo aliketi mtu huyo, akaangalia upande wa pili wa meza na kuniambia jambo fulani, na kusema kweli, ni—ninge—ningetoa, leo, dola mia tano kama ningeweza, kama kamwe sikuhudhuria chakula hicho cha jioni. Mnaona? Maana sikuzote nimemheshimu sana mtu huyo, na hapo kile nilichoona! *Tsk*! Mnaona? Ni. . .

40 Unafikiri hili ni rahisi, ndugu, hutambui, hutambui tu ni nini, ina—inaua, na kiasi chake kidogo tu. Unazungumza tu na mtu fulani unayemjua, kuhusu ninii yao—kuhusu hali yao, ama kitu kama hicho, ni kama tu. . .

41 Unaona, hutambui, bali wewe ndiwe unayeleta maono hayo, si mimi, ni wewe. Nisingeweza kufanya jambo hilo, mimi. . . ni. . .silidhibiti, linanidhibiti. Sasa, ninii tu. . .(Naweza kupata kama dakika tano za ziada? Nafikiri ingesaidia mkutano wetu, mnaona.)

42 Niwaambie nini, mnaona, tunakuja kwenye ibada ya uponyaji. Sasa angalieni, sisi sote ni wavulana wadogo, nasi tunashuka kwenda kwenye sarakasi, sikukuu kubwa inakuja mjini, ama, sarakasi, sisi sote. Vema, inatukia kwamba, mimi ni jamaa mkubwa mno, mwembamba, mrefu, na—nami ninatembea, nanyi ni jamaa wafupi, wanene, wazito. Vema, twendelee mbele, tutaingiaje? Iko nyuma ya ua wa ubao. Vema, inatukia kuwa, ninaangalia *hapa* juu, na hili hapa shimo la kifundo *hapa* juu. Vema, ni—ninasema. . .

Wanasema, "Aisee, Ndugu Branham, kuna nini mle ndani?"

"Vema, hebu ruka juu uone."

"Loo, kamwe nisingelifikia."

43 Mnaona, hatuna budi kuwa jinsi tulivyo, "Karama na miito havina majuto." Ulipozaliwa katika ulimwengu huu, kabla ulimwengu haujaanza, Mungu alikujua, akakuweka mahali pako. Kama sivyo, basi Biblia sivyo ilivyo. Hiyo ni kweli kabisa. Mungu aliweka majina yetu kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, si wakati ulipokuja madhabahuni, bali kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, hiyo ni kweli, hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Hiyo ni kweli.

44 Mwana-Kondoo alichinjwa lini? Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Na wakati Mwana-Kondoo alipochinjwa, jina lako liliandikwa kwenye Kitabu Chake. Mungu, kwa kujua Kwake tangu zamani, aliona mambo yote, Yeye hana kikomo, Yeye alijua mwisho tangu mwanzo. Hataki mtu yeyote apotee, hiyo si shauku Yake, bali akiwa ni Mungu, ilimbidi ajue ni nani angepotea, na ni nani asingepotea. Unaona? Kama vile Esau na Yakobo, Yeye alimchukia mmoja, na kumpenda huyo mwingine kabla hata hawajazaliwa na kupata nafasi ya kufanya chochote, kwa sababu Yeye alikuwa Mungu, alijua mambo yote.

45 Sasa mnaona, na karama na mwito havina majuto. Yesu asingeweza kujizuia kuwa Mwana wa Mungu, Yeye alikuwa—Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu, aliyekusudiwa tangu zamani, aliyechaguliwa tangu zamani kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, na hata aliuawa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mnaona? Hiyo ni kweli.

46 Isaya alimwona Yohana Mbatizaji miaka mia saba na kumi na miwili kabla hajazaliwa, ndipo akasema, "Yeye ni sauti ya mtu aliaye nyikani." Um-hum. Hiyo ni kweli? Asingeweza kujizuia kuwa Yohana Mbatizaji, alikuwa ni Yohana Mbatizaji kwa sababu Mungu alikuwa amemchagua Yohana Mbatizaji.

47 Ninaamini ilikuwa ni nabii Ezekieli, ama, Yeremia, Yeremia, ninaamini ndiye, nabii, ninaamini Yeremia 1:4, alisema, "Mimi, kabla hata hujachukuliwa mimba wala kuumbwa katika tumbo la uzazi nalikujua, nikakutakasa, na kukuita na kukuweka kuwa nabii kwa mataifa," kabla hata hajaumbika katika tumbo la mama yake, hakika. Mnaona? Mungu ameweka kanisani, kwanza mitume, manabii, na kadhalika.

48 Sasa, hizo karama, ambapo Paulo alisema, "Mimi . . . Ombeni kwa bidii kwa ajili ya karama zilizo bora zaidi," hizo ni karama za kanisa, hizo si ofisi. Kuna *karama*, halafu *ofisi*. Kuna ofisi, hiyo ni nabii. Kuna tofauti kubwa sana kati ya *nabii* na *karama ya unabii*. Kabla ya karama ya unabii kweli kutolewa kanisani, haina budi kuja mbele ya wapambanuzi wawili au watatu walio na ka—karama ya upambanuzi, kusema kama hata inaweza kunenwa, lakini kamwe hamkuona mtu yeyote akisimama mbele ya Isaya kuamua, mnaona, yeye alizaliwa nabii. Lakini hao manabii, walikuwa . . . walikuwa na BWANA ASEMA HIVI moja kwa moja maishani mwao. Mnaona? Mnaona, kuna tofauti nyingi sana.

49 Kile ninii, loo, nafikiri kile kanisa linachohitaji ni masomo mazuri sana, ya Kimaandiko juu ya mambo, ndipo hakuna kukosea. Mtu akisimama na kunena kwa lugha, mmoja anatoa tafsiri . . . Sasa, mimi si hakimu, la, lakini kwa upambanuzi unaweza kujua, baadhi yake ni mwili kabisa, wanasema, "Tazama Yeye yuaja. Tazama Yeye yuaja," na kitu kama hicho,

mbona, hakika, sote tunajua hilo, Mungu alisema, "Msipayuke-payuke," akatuambia tusipayuke, wala asingefanya hivyo.

50 Wakati kanisa letu, wakati walipotoa moja ya hizo, wakati nilipoendeleza kanisa langu, wakati nilipokuwa Mpentekoste kwa mara ya kwanza, kama unabii ulitolewa, watu wote wenye karama walikutana kwanza, nao wakatumia . . . Wao ni sehemu ya kanisa. Walitoa, tuseme, kama mtu alinena kwa lugha, na mwingine akatoa tafsiri, ilibidi liwe ni jambo fulani moja kwa moja kwa kanisa, ilibidi iwe ni ujumbe, "Mwambie Ndugu *Fulani-wa-fulani* aondoke kwenye *hili*, wala usifanye *hivi*; ama usiwe kwenye kona *hii* wakati *huo*, maana jambo fulani litatukia," halafu basi kabla jambo hilo halijatolewa wakati huo, ilibidi lipambanuliwe na wapambanuzi wawili au watatu mbalimbali, nao wakaandika majina yao kwenye karatasi na kuiweka kwenye dawati langu, nami nikalikabidhi kanisa. Kama lilitendeka, Mungu ashukuriwe; kama halikutendeka, nisingewaacha wafanye hivyo tena mpaka walipomwondoa huyo pepo mchafu kutoka kwao. Hiyo ni kweli, hiyo ni kweli.

51 Haitubidi kuchukua kibadala, anga za Kipentekoste zimejaa yaliyo halisi. Kwa nini uchukue kitu ambacho ni bandia wakati kuna kilicho halisi hapo? Bila shaka. Lifanye halisi, ndipo hakuna kukosea. Mnaona, mmelipata papo hapo.

52 Mtu fulani alisema, kama, "BWANA ASEMA HIVI: Mwambie Ndugu Branham, usiku wa leo kutakuwako na mwanamke atakayeingia, anatoka Ohio, angekuwa amevaa vazi fulani, ana kansa. Lakini alipokuwa msichana mdogo, aliiba pesa kutoka kwenye hazina, kamwe hawezi kuponywa. Mwambie—mwambie aende arudishe pesa hizo, na asahihishe jambo hilo, BWANA ASEMA HIVI, ataponywa." Hilo hapo. Kama hakukuwa na ujumbe wa moja kwa moja kwa mtu kama huyo, ulikuwa ni mwili, hatukuukubali hata kidogo.

53 Vipi kama nikija hapa na kusema, "Bwana ananiambia mtu fulani ana ugonjwa wa figo. Ni wangapi wana ugonjwa wa figo?"

54 Hakika, ni kote jengoni. Nimeona karama hiyo ya Mungu ikiigizwa sana.

55 "Mtu fulani ananiambia, Bwana ananiambia, haleluya, ninahisi, ni wasiwasi, mtu fulani humu ndani ana wasiwasi."

56 Hakika, umati wote uko hivyo. La, hilo silo. Ni nani? Nao walitoka wapi? Ni kitu gani kilichousababisha? Na matokeo yake yatakuwa nini? Mnaona? Huo ni uigaji wa kimwili, ambao ni wa kimwili machoni pa Mungu.

57 Kwa nini ukubali huo wakati kuna ulio halisi? Kwa nini ufanye hivyo wakati kuna wa kweli? Kwa hiyo, jambo ndilo hili, mnaona, kisha unyoshe mkono juu kabisa, na kuvuta juu, hiyo ndiyo karama, mnaona, mtu aliyesimama pale. Mnaona?

Ninaangalia juu, nasema, "*Huff!* Nilimwona twiga."

"Loo, ulimwona?"

58 Sasa, mnajua hiyo ni nini? Katika mambo ya kawaida, sasa, ninawaonyesha mfano, katika mambo ya kawaida, sasa, mnaona, labda hao ndugu wengine, wangeweza kubeba maji, wana nguvu, lakini ilitokea kwamba nilizaliwa nikiwa mrefu. Mungu hutufanya kile tulicho, wahubiri, wainjilisti, mitume, manabii, Mungu aliweka kanisani. "Ni nani akijisumbua aweza kujiongezea kimo chake hata mkono mmoja?" Huwezi kufanya hivyo. Usijaribu kuwa *huyu* wakati wewe ni *yule*, unaona, kuwa tu kile ulicho.

59 Sasa, ni kitu gani kinachofanya hivyo? Hiyo ni wewe mwenyewe unayefanya hivyo, unaona. Kuinuka, "*Huff!*" Karibu kunaniua. Kasema, "Loo, ni, ni—nilimwona twiga."

"Uliona nini tena?"

"Loo, jamani!" Mimi huyo ninaenda tena, ninaruka juu, "*Huff!* Ndovu."

"Loo, ulimwona?"

60 Mnaona, sasa hiyo ni jukwaani, hivyo ndivyo unavyoitumia karama ya Mungu. Hilo ndilo jambo lile lile alilofanya yule mwanamke aliyegusa vazi Lake. Mnaona? Kamwe hakusema, "Nilifanya *hivi-na-vile*." Alisema, "Imani yako imekuokoa." Unaona? Aliangalia kote, akagusa vazi Lake, na kusema, "Naona nguvu zimenitoka." Akaangalia kote kwenye kusanyiko mpaka akamwona, na kusema, "Loo, imani yako imekuokoa." Unaona? Akasema, "Mimi . . . "

61 Lakini sasa angalieni, wakati Baba alipomwonyesha ya kwamba Lazaro atakufa . . . Sasa, kumbukeni, Yesu kamwe hakufanya jambo moja bila Baba kumwonyesha Yeye kwanza. Ni wangapi wanaojua hilo? Yohana Mtakatifu 5:19: "Amin, amin," hiyo ni *kabisa*, *kabisa*, "nawaambia, ya kwamba Mwana hawezi kutenda neno, mpaka amwone Baba analitenda kwanza." Hiyo ni kweli.

62 Kwa hiyo Baba alimwambia, "Nenda zako sasa, kwa sababu Lazaro atakufa, na baada ya siku nne, ama, siku *kadha*, urudi, Nami nitakufanya Wewe umfufue tena." Mnaona?

63 Vema, Yeye aliondoka, kamwe hakusema mahali alipokuwa anaenda. Lazaro akashikwa na ugonjwa, wakatuma mtu Kwake, na mbona, akaendelea mbele tu, mnaona; wakatuma mtu Kwake tena, akaendelea mbele tu, akapuuza. Hilo lilikuwa ni jambo geni Kwake, mnaona. Lakini watu wanaongozwa na Roho wa Mungu, kuwa—kuwa tu na imani na uamini. Wana—wanafuata ono, hawawezi kukwambia la kufanya, waache tu.

64 Kwa hiyo basi, wakaja kugundua, ndipo baada ya Yesu kujua wakati ambao Baba alikuwa amemwonyesha ulikuwa umetimia, akasema, "Rafiki yetu Lazaro amelala."

Akasema, "Vema, iwapo analala, anafanya vema, mwacheni. Vema, hilo ni sawa."

Akasema, "Amekufa. Na kwa ajili yenu nina furaha sikuwapo, lakini ninaenda kumwamsha."

65 Mwangalieni kaburini, "Baba, ninakushukuru, Wewe tayari..." mnaona, "lakini nilisema jambo hili kwa ajili ya hao waliosimama karibu," ili tu kutoa mfano. Ndipo akamwita Lazaro kutoka kaburini na kumfufua mtu kutoka—kutoka katika usingizi wake wa mauti, aliyekuwa kaburini siku nne.

66 Na siku nne pua tayari imebonyea, mnajua hilo, nyumba ya maiti...uharibifu umeingia mwilini. Ndipo akaita roho ya mtu huyo irudi, akamfufua, kisha akaenda kula chakula cha jioni pamoja naye. Akaishi, hiyo ni kweli, wala Yeye kamwe hakusema jambo moja kuhusu kuwa dhaifu, lakini yule mwanamke aligusa vazi Lake, ndipo nguvu zikamtoka. Mnaona? Hapo ni wakati Baba alipokuwa anatumia karama Yake.

67 Sasa, hivyo ndivyo ilivyo katika huduma hii, ninaweza kuwa katika chumba changu cha hoteli, Roho Mtakatifu atasema, ama mahali fulani nyumbani, ama popote pale, "Panda kwenye ndege uende mahali fulani, ushuke uende mahali fulani, utapata mahali fulani pa kuingia," namna hiyo, na mambo makuu yanatukia; namna hii, mnaona gazetini kuhusu jambo hilo, hakuna mtu aliyepata kujua ni nani aliyefanya hivyo, hawajui bado, hiyo ni kweli.

68 Huko Denver wakati huo, hapo ni wakati Roho Mtakatifu aliponiita nitoke, yule mtu aliyekuwa na TB, na kuniambia nisimame pale pembeni mwa lile duka la malimali mpaka mtu huyo ashuke na Biblia hiyo mkononi mwake kwenye kile kiti cha magurudumu. Kasema tu: "Jambo la Ajabu Limetukia: Mtu Ameponywa Kwenye Kiti Cha Magurudumu, Kisha Mtu Anatoweka." Sikutoweka, nilipitia moja kwa moja kwenye hilo duka la malimali, nikatoka huko nje kichochoroni, na kuendelea, moja kwa moja, uwanja wa ndege. Hiyo ni kweli kabisa. Mnaona?

69 Lakini kamwe hawakujua ilikuwa ni nini, mambo hayo. Kwa sababu, mnaona, si...Inaleta faida gani? Mnaona, Mungu hupata utukufu, na maadamu, tunajaribu kujitwalia utukufu ndani ya mwanadamu, basi mmekosea kabisa. Hiyo ndiyo sababu siwaiti watu na kuwawekea mikono, niseme, "Upokee, ndugu, *hili* ndilo *lile*." Hilo ni sawa, lakini hilo linaweka mengi kupita kiasi, useme, "Ndugu Branham aliniwekea mikono. Utukufu kwa Mungu, nikapona."

70 Hebu *Ndugu Branham* asiwemo. "Nilimwona Bwana Yesu Kristo, Naye akaniwekea mikono Yake. Niliweka mkono wangu juu Yake, hata sikuwa kwenye mstari wa maombi, niliketi tu pale na kuamini, Naye akamgeuza Ndugu Branham na kusema *hivi-na-hivi*." Haya basi. Jambo ndilo hilo, hilo ndilo jambo lenyewe. Mnaona? Sasa, angalieni hiyo ndiyo tofauti basi.

71 Sasa, ninapoenda juu kusema, “Huyu hapa mwanamke amesimama hapa,” naye anasema. . .nasema, “u hali gani?” ninajaribu kufanya nini? Kama vile Yesu alivyozungumza na yule mwanamke kisimani, akijaribu kuwasiliana na roho yake. Mnaona?

Naye anasema, “U hali gani?” Mnaona, ninashika roho yake basi.

72 Dakika chache zake, mtetemo wa ajabu kutoka kwake, ama kitu kigeni, mimi, “Loo-loo, huyo ni—huyo ni—huyo ni mtu fulani anayejaribu kuvuta kitu fulani, sasa ngoja kidogo tu,” angalieni kitakachowapata, angalieni tu jinsi watakavyomwondosha jukwaani katika muda mfupi. Mnaona?

73 Ni—ninasema, “U hali gani?” Naongea nao, ninaanza kusema jambo fulani, mwajua, na muda si muda mwajua, kama halionekani sawa, ninangojea tu basi, nione kile Roho Mtakatifu asemacho. Mnaona?

74 Halafu basi, kama vile jamaa fulani alivyokuja kwenye mstari wa maombi, akajifanya, alidhani ilikuwa ni telepathia, maana aliandika kwenye kadi ya maombi, aliandika hapo alikuwa na TB, na kila kitu, akaja, mstarini, akasema—akasema, “U hali gani?”

75 Nami nikasema, “U hali gani, bwana?” Naye akasema. . . Nikasema, “Vema, unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake?” Mnaona, hivyo ndivyo Malaika alivyosema, “Wafanye watu wakuamini.”

“Naam, bwana.”

76 Wala hilo halikusikika sawa, halikukolea. Mnaona, mimi mwenyewe ningeninii. . .mbona, alikuwa ni mtu mwenye sura nzuri, jamaa mwenye sura nzuri tu. Nikasema, “Naam, bwana.” Nikaanza kuzungumza naye, nikasema, “Huna shida yoyote, wewe ni mzima kabisa.”

Kasema, “Umekosea.”

Nami nikasema, “La, sijakosea.”

Akasema, “Chukua kadi hiyo ya maombi hapo chini, na uangalie,” kasema, “Nina TB, kansa,” yote, yote aliyokuwa ameandika.

Nikasema, “Sijali ulicho nacho kwenye kadi hiyo ya maombi,” nikasema, “huna shida yoyote.”

Akasema, “Vema, nimeandika kwenye kadi yangu ya maombi.”

Nikasema, “Hilo halidhuru. . .Sijali ulichoweka kwenye kadi yako ya maombi, hilo halimaanishi kitu, mnaona, ni yale Roho Mtakatifu asemayo.”

Naye akasema, “Vema, ni. . . ”

Nikasema, "Vema, labda ulikuwa na imani ya kutosha kuponywa kabla hujaja mkutanoni. Mimi . . . "

Akasema, "Na hivyo ndivyo ilivyo!"

77 Ndipo nikawaza, "Ni nini kinachoendelea hapa?" Alionekana kana kwamba alikuwa Mkristo. Nikaangalia pande zote, hapo nikaangalia ukutani, kama upande *huu*, na hapo nikaliona, likitoka nje. Basi nikamgeukia, wengi wanaoketi hapa sasa walikuwa moja kwa moja mkutanoni wakati lilipotukia, basi ni—nikasema, "Kwa nini—kwa nini umruhusu ibilisi aweke kitu kama hicho niani mwako?" Nikasema, "Sasa, wewe ni wa kanisa fulani," sitalitaja jina hilo, "ambalo halininii . . . linaamini siku za miujiza zimepita. Nawe ulikuwa mkutanoni hivi majuzi usiku na kuniambia, na—na kusema moyoni mwako, hasa, kwamba hii haikuwa kitu ila telepathia ya kiakili."

78 Ndipo nikasema, "Mtu huyo aliyeketi papa hapa kwenye roshani amevaa tai nyekundu, suti ya kijivu, wewe ulikuwa nyumbani kwake hivi majuzi usiku, ulikuwa umeketi kwenye meza iliyokuwa imefunikwa kitambaa *hivi*, nawe ukaamua moyoni mwako kwamba utashuka uje hapa na kuandika hayo kwenye kadi yako ya maombi, uje hapa."

Ndipo mtu huyo akapaza sauti na kusema, "Hiyo ni kweli iliyo hai," akiketi jukwaani, namna hiyo.

79 Nami nikasema, "Kwa sababu umesema, na kuweka huo kwenye kadi yako ya maombi, sasa unao." Naye akafa yapata majuma sita baadaye. Um-hum.

80 Mnaona, hatuigizi kanisa, tunaishi katika Uwepo wa Roho Mtakatifu. Mnamkumbuka Anania, Safira, afadhali uwe mwaminifu, na uwe sahihi na Mungu kabla hujajaribu hilo. Kumbukeni, "Ni jambo la kutisha kuanguka mikononi mwa Mungu aliye hai." Mnaona?

81 Huo hapo, ukaja moja kwa moja juu yake, nao ubainishaji wa huo ugonjwa na kadhalika, ulionyesha alikuwa na kansa na TB pia. Alisema hilo, yeye, na maneno yake yakatimia, hiyo ni kweli kabisa, alitia muhuri maangamizi yake mwenyewe, vivyo hivyo hasa.

82 Kama vile Daudi alivyofanya wakati aliposimama mbele ya Nathani, na kusema, "Mtu huyo hakika atakufa." Mnaona, itambidi kulipia hilo, mnajua kile Nathan alichomwambia, alitia muhuri maangamizi yake mwenyewe. Kwa hiyo, bado ni Mungu yule yule, sisi—sisi hatumtumikii Mungu mwingine wa kutoka siku nyingine. Sasa, hivyo ndivyo ilivyo, kwa hiyo mwamini tu Mungu.

83 Sasa, kwa kama dakika kumi ninataka kumalizana na *Yehova-Yire*. Je, mko tayari kungojea kwa dakika chache tu? Mko tayari? Vema, najua ninyi ni . . . Maharagwe hayataungua, na yakiungua, hayata—hayataninii . . . hili—hili litawasaidia.

84 Sasa, jana usiku tulimwacha, Yehova-Yire, baraka, Ibrahimu na Sara, na alikuwa amewapa ile—ile ahadi ya yule mvulana mdogo, na alikuwa amewageuza wakawa kijana mwanamume na mwanamke. Mnaamini hilo? Hakika, ilimbidi kufanya jambo fulani kumtia nguvu, kwa hiyo akamgeuza tu, maana ilionyesha, sifa zenyewe za kile alichofanya zilionyesha ya kwamba alikuwa kijana, mwanamke mrembo tena.

85 Basi kumbukeni, hebu niwaonyeshe jambo fulani, Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka mia moja, naye akaishi akawa na umri wa miaka mia na sabini na mitano, na baada ya miaka arobaini, baada ya Isaka kuwa na umri wa miaka arobaini, Ibrahimu alioa mwanamke mwingine na akawa na wana saba mbali na mabinti. Amina. Hakika, alifanya hivyo. Hiyo ni kweli? Kwa hiyo, mnaona, Yeye alimgeuza kuwa kijana mwanamume, akamgeuza mama kuwa kijana. Hivi hamna furaha kwamba ninyi ni watoto wa Ibrahimu? Hivyo ndivyo atakavyotufanyia siku moja katika Kuja Kwake.

86 Sasa angalieni, upesi sasa, tutataja hoja zake muhimu kama tukiweza. Sasa, tunaona ya kwamba mara baada ya jambo hilo, maskini huyo Isaka alizaliwa. Mungu akamgeuza akawa msichana wa kupendeza sana, naye akawa kijana mwanamume, ndipo mtoto Isaka akazaliwa. Ndipo basi Isaka alipofikia umri wa kama miaka kumi na miwili. . . Ninawazia mvulana mdogo, mzuri wa Kiyahudi. Basi hiyo ilikuwa ni hisia ya jinsi gani kwa huyo mama na baba, baada ya miaka hii yote kupata hakikisho!

87 Mungu anapojibu maombi kwa ajili yako wakati mmoja, basi unajua ya kwamba Yeye ni Mungu anayejibu maombi. Hiyo ni kweli? Sasa, ni wangapi hapa wamempokea Roho Mtakatifu? Inueni mikono yenu, wote walio na Roho Mtakatifu. Sasa, ungewezaje kutilia shaka uponyaji? Ni wangapi hapa waliopata kujibiwa maombi? Hebu tuone. Hakika. Basi Yeye ni Baba anayejibu maombi, sivyo? Haya basi. Mnapata hilo wazo? Kama unahitaji chochote, omba. Umekosa hekima, mwombe Mungu, unaona, Yeye atakupa.

88 Sasa, Ibrahimu alijua ya kwamba alikuwa ameshikilia ahadi hiyo, Naye alikuwa ameitimiza. Mnaona? Kwa hiyo, mnaona mvulana huyo mdogo alizaliwa.

89 Kwa hiyo, Bwana akasema, "Sasa, nitawafanya hao watu huko chini katika Assemblies of God huko chini Long Beach, yapata miaka elfu mbili na mia tano tangu sasa, nitawapa hakikisho halisi, basi Uzao wote wa Ibrahimu ujue ya kwamba—ya kwamba mimi ni Mungu anayejibu maombi, nami ninawatimizia watu Wangu ahadi Zangu."

90 Kwa hiyo Yeye akasema, "Nitamchukua Ibrahimu, kwa sababu ninajua ananiamini Mimi, nami nitauliza. . . Tayari nimemwambia ningemfanya baba wa mataifa, alingojea miaka ishirini na mitano, mpaka sasa ana umri wa kama miaka mia

moja na arobaini na mitano, ama, umri wa miaka mia moja na kumi na miwili," mahali fulani namna hiyo, "sasa nitamwambia amchukue mvulana huyu mdogo ambaye amemngojea, na kumchukua na kumwua. Ibrahimu atanitii Mimi."

91 Sasa, hilo lilikuwa jaribio la jinsi gani kwa Ibrahimu! Wazia hilo lilikuwa ni nini. Sasa tuko katika Mwanzo 22. Sasa, kwa kuwa hakutaka, labda, hakutaka kumwambia Sara, hakutaka kwenda na kumwambia, "Sara, ninaenda kumwua Isaka asubuhi ya leo," la, hakutaka kufanya hivyo, kwa hiyo aliamka tu mapema, na kukata kuni, akazipasua, Maandiko yanasema, akaziweka kwenye, labda kwenye gunia dogo la namna fulani, na kuziweka mgongoni mwa nyumbu, akamchukua mtumwa, akamchukua Isaka, wakatembea mwendo wa siku tatu.

92 Sasa, mtu yeyote, ninaweza kutembea siku yoyote, maili thelathini, nilizoea kufanya doria, nilitembea miaka saba maili thelathini na thelathini na tano kila siku kupitia nyikani, na sasa tuna miguu ya petroli. Na watu katika siku hizo ambapo iliwabidi kutembea kila mahali waendako, Ibrahimu angeweza labda, katika hali yake ya ujana wakati huo, labda angeweza kutembea maili mia moja, rahisi, katika siku tatu.

93 Sasa, angalieni, kutoka kwenye ustaarabu, yuko huko nyuma siku tatu, ndipo akainua macho yake na kuona mlima ukiwa mbali sana, ambapo Bwana alimwonyesha. Sasa angalieni mahali alipoenda.

94 Sasa, basi alipokaribia pale, aliwasimamisha maskini hao nyumbu, na kuwafunga, akachukua kuni na kuziweka begani mwa Isaka. Naye akasema . . . Sasa sikilizeni hili, loo, hili ni zuri sana! Ni . . . Laiti tungalikuwa na wakati mwingi juu ya jambo hili. Mnaona? Linapendeza sana! Akasema, "Ninyi ngojeni hapa pamoja na nyumbu; mimi na kijana tutaenda kule kuabudu, kisha tutarudi."

95 Atarudije? Anaenda kumwua. Atarudije? Lakini kile ninii . . . Tuchukue katika Waebrania pale, kama tungalikuwa tu na, ama, katika Warumi mlango wa 4, kama tu tungalikuwa na wakati wa kulipitia! Lakini Ibrahimu alisema hivi moyoni mwake: "Nilimpokea kama mtu kutoka kwa wafu, nami nina hakika kabisa ya kwamba Mungu anaweza kumfufua kutoka kwa wafu."

96 Mfano mkamilifu wa Mungu akimtoa Mwanawe wa pekee, mnaona. Ibrahimu akimtoa Isaka sadaka, Mungu akimtoa Mwanawe, na kutoa hakikisho, kwa sababu Mungu alikuwa tayari amemwambia, "Nimeninii, nimekufanya baba wa mataifa." Sasa, tayari alikuwa amempa ile ahadi, naye alijua bila shaka hata kidogo, kwamba atakuwa, tayari alikuwa. Sio "Nitafanya," "Nimefanya, tayari nimefanya hivyo."

97 Na hivyo ndivyo uponyaji wako ulivyo, Yeye tayari ameufanya, kuna jambo moja tu lililosalia kwako kufanya,

kulikubali. Hivyo ndivyo ilivyo na wokovu wako, kuna jambo moja tu la kufanya, kulikubali.

98 Nikisoma makala hayo asubuhi ya leo ya *Mwandishi Wa Kibaptisti*, wakati ndugu huyo alipokuwa akitoa, nilimwona yule mhubiri wa Kibaptisti akisimama na kuiangalia, akaiangalia sawasawa usoni, akasema, "Ninataka hiyo baraka ya Kipentekoste." Mungu hana upendeleo, kwa maneno mengine. Naye akaipokea. Naye alikuwa na mikutano mikubwa huko Chicago pamoja na Moody, naye alikuwa mhudumu mashuhuri sana wa Kibaptisti.

99 Kwa sababu kama Mungu anakujulisha, kwamba ni kwa ajili yako, basi ni yako, ni mali yako. Kama wewe ni mwenye dhambi, na kitu Fulani kinasema, [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] "Mimi ni Bwana nikuokoaye," hiyo ni Sauti ya Mungu, geukeni, isikilizeni, muikubali na msonge mbele. Yeye asipobisha kamwe, mbona, kamwe huwezi kuja. Kwa hiyo, si yule atakaye, wala yule apigaye mbio, ni Mungu arehemuye. Hiyo ni kweli. Mnaona, Mungu akibisha moyoni mwako, hayo ndiyo majaliwa makuu kuliko yote uliyopata kuwa nayo maishani mwako mwote, mtu yeyote aliyepata kuwa naye, ni Mungu kukupa mwaliko wa kumjia Yeye.

100 Sasa, tunaona ya kwamba Ibrahimu alikuwa na imani, maana alikuwa amemngojea mtoto huyo miaka ishirini na mitano, na sasa Mungu anamwambia amchukue mtoto yuyo huyo na kumwua. Sasa, hilo lilikuwa jaribio la jinsi gani! Lakini Ibrahimu hakusita katika ahadi ya Mungu, alisema, "Kama Mungu akinipa huyu kutoka kwa wafu, Mungu anaweza kumfufua kutoka kwa wafu, ninaendelea moja kwa moja, maana Yeye aliniambia nilikuwa baba wa mataifa."

Sasa ninamwona ibilisi akijaribu kukaa begani mwake, na kusema, "Ibrahimu, kama . . . unajua unampenda Mungu."

"Loo, naam, nampenda Mungu."

101 "Vema basi, kama unampenda, unaangamizaje u—ule ushahidi wenyewe na kitu pekee kinachoweza kuwa, kwamba utakuwa baba wa mataifa?" Mnaona? "Utafanyaje hilo? Utakuwaje baba wa mataifa kama ukiangamiza ninii yako . . .? Uzao pekee ulio nao ni mvulana huyu aliyeahidiwa kupitia kwa mwanamke huyu. Na sasa, utafanyaje jambo hilo?"

"Vema, kama Mungu aliniambia nilikuwa baba wa mataifa, hiyo ni juu Yake kufanya hivyo. Mungu alisema hivyo, na hilo latosha."

Mnapata hilo wazo? "Nitakuwaje, nitaponywaje kama daktari akiniambia nitakufa?"

Mungu alisema hivyo, na hilo latosha. Hilo ndilo wazo.

“Nitafanyaje jambo *hili*?” “Ninawezaje kupanda juu angani na kuona kitu *fulani*, nacho kitashuka chini, elementi, na kuniponya?”

102 Si—sijui. Uliunyoshaje huko juu na kupata *kitu* kilichokuokoa? Jambo ndilo hilo. Unaona, hiyo ni kuu kuliko uponyaji, ni kuu sana kuliko uponyaji, maana inabadilisha tabia yako yote, inabadilisha nia yako, inabadilisha mawazo yako, inabadilisha kila kitu ndani yako, kwa hiyo ni kuu zaidi namna hiyo.

103 Sasa, lakini Ibrahimu alimwamini Mungu. Sasa, angalieni yaliyotukia. Loo, nafikiri hili ni zuri. Sasa angalieni, Ibrahimu hakubeba kuni mwenyewe, aliweka kuni juu ya mgongo wa Isaka, mnaona, ikionyesha tu ya kwamba miaka mia chache baadaye, ya kwamba Kristo, yule Uzao wa kweli wa Ibrahimu, angebeba gogo Lake Mwenyewe la dhabihu kuelekea Golgotha. Unapomwona Yesu akipanda kwenda Golgotha, ama, ninamaanisha Ibrahimu na—na mwanawe mdogo, Isaka, wakipanda juu, naye Isaka akibeba kuni hizi, hicho kilikuwa ni kivuli cha Yesu Kristo akipanda kwenda Golgotha, akienda kwa dha-. . .mtiifu.

104 Na, mwajua, mtoto Isaka akaanza kushuku, naye akasema, “Baba,” akasema, “tuna moto hapa, tuna kuni hapa, tuna kila kitu tayari, lakini yuko wapi mwana-kondoo, sadaka ya kuteketezwa? Iko wapi?” Akaanza kuangalia kote, “Ninaona kila kitu ila kitu kimoja.” Loo, jamani! “Itakuwaje?”

105 Basi angalieni sauti yenye nguvu ya Ibrahimu, jinsi alivyomjibu mwanawe, mnaona, hakuninii, labda, hakujua alilosema, alisema, “Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka ya kuteketezwa.” Mungu atajipatia. *Yehova-yire*, “Bwana atajipatia Mwenyewe dhabihu.” Loo, napenda hilo, nanyi je?

106 “Nitafanyaje jambo hilo, Ndugu Branham? Nimepitia mistari ya maombi, nimefanya *hivi*, nimefanya *vile*. Ninawezaje kufanya hivyo?”

Mungu atajipatia.

“Utaepukaje jambo hili? Unasema hivyo, unajua unajifanya mwenyewe shabaha? Mimi . . . ”

Lakini Mungu atajipatia. Hivyo tu.

“Unajuaje unaposimama jukwaani hivi . . .?”

107 Mungu atajipatia. Hayo tu ndiyo nijuayo. Yeye aliahidi jambo hilo, tunalichukua Neno Lake, tunaliamini. Hilo latosha, hivyo tu, liondokee. Maana Mungu alisema hivyo, hiyo ni, haina budi kuwa hivyo.

108 Wawili hao wakaondoka pamoja wakapanda mlimani, hatimaye wakafikia mahali, akabingirisha mawe pamoja, akazipanga zile kuni. Basi mwangalieni mtoto Isaka, mtiifu hata

kufa, kama Kristo alivyokuwa. Akaivuta mikono yake nyuma yake, akaifunga, akafunga miguu yake, naye akamlaza maskini mvulana huyu pale, mwanawe wa pekee, yule uzao aliyepaswa kuwa wa ahadi, akamlaza juu ya madhabahu, akazipapasia maskini nywele zake nyuma kutoka usoni mwake, mvulana mdogo, mwenye sura nzuri. Mama atasema nini utakapofika nyumbani na kusema kwamba ilikubidi kumwua mwana huyo? Lakini Mungu atatoa, maadamu tu unalitii Neno Lake.

109 Akakitupa maskini kichwa chake nyuma namna *hiyo*, akaunyosha mkono kifuani mwake, akatoa ki. . . kisu kutoka kwenye ala yake, kisha akakiinua juu namna *hiyo*, akavuta nywele zake nyuma namna *hiyo*, na moyoni mwake akihema kwa nguvu, na kumeza tena pumzi, ni kusema, "Kwaheri, Isaka, mwanangu," akainua mkono wake, na yapata wakati huo, katika utii mkamilifu, hata kama unafanya jambo baya na kutembea katika utii, Roho Mtakatifu yupo hapo kukuzuia.

110 Unasema, "Nahofia kama kamwe nikimpokea Roho Mtakatifu, huenda nikatenda yasiyofaa."

111 Usijali, kama ni Roho Mtakatifu, Yeye atajua wakati wa kukusimamisha, na wakati wa kukuanzisha, Yeye ana kitufe mkononi Mwake, unaona, kwa hiyo anajua wakati wa kufungulia na kuzima, jisalimishe tu kwenye rehema Zake.

112 Hivyo ndivyo unavyofanya na uponyaji, unajisalimisha kwenye rehema Zake, Yeye aliahidi jambo hilo, ni Neno Lake, hana budi—hana budi kulitimiza Neno Lake, kama sivyo, Yeye si Mungu.

113 Kwa hiyo tunaona basi, mara tu alipoanza kumchoma kisu maskini mwanawe afe, hapana shaka Roho Mtakatifu alimshika mkono, kasema, "Ibrahimu, Ibrahimu! Zuilia mkono wako, najua sasa kwamba unamcha Mungu, najua ya kwamba unanipenda Mimi."

114 Basi nini kilitukia? Yapata wakati huo, akasikia kitu fulani nyuma yake, na kulikuwa na kondoo mume, huyo ni kondoo dume, aliyenaswa vichakani kwa pembe zake.

115 Sasa nataka kuliuliza hili darasa jambo fulani katika kufunga: Huyo kondoo dume alitoka wapi? Alikuwa ameyabingirisha mawe kila mahali pale, na kutengeneza madhabahu, na kupanga kuni, na kila kitu, alitokea wapi? Alikuwa angalau maili sabini na tano hadi mia moja kutoka kwenye ustaarabu, safari ya siku tatu, kuna simba, mbweha, wanyama mwitu wakali sana wa kila namna mle ndani, wangewala tu kondoo, na vitu kama hivyo. Asingeweza kunusurika, hakuna ustaarabu mle. Huyo kondoo dume alitoka wapi?

116 Sasa, jambo lingine, yeye yuko huko juu kabisa mlimani ambako hakuna maji. Angewezaje kamwe kufika kule? Ilikuwa ni kitu gani? Kwamba. . . hili fungu linaelezea hilo, Yeye ni

Yehova-Yire, Yeye alinena huyo kondoo dume akawa. Sasa, halikuwa ono, ono halitoki damu. Alienda akamchukua huyo kondoo dume, akamweka juu ya madhabahu, na kukata koo yake, ndipo damu ikamtoka. Halikuwa ono, ilikuwa ni kondoo dume.

117 Na hiyo ndiyo sababu Ibrahimu akapaita mahali hapo *Yehova-yire*. Kama Mungu ametoa ahadi, Mungu anaweza kutoa kitu kwa ajili ya ahadi hiyo. *Yehova-yire*, "Bwana atajipatia Mwenyewe." Kondoo dume huyo alinenwa akawa katika dakika moja, hiyo dakika nyingine hakuweko tena, bali ilitimiza kusudi la Mungu.

118 Naye Mungu anaweza, asubuhi ya leo, kumtuma Roho Mtakatifu miongoni mwetu, Yeye anaweza kutuma nguvu za kuwaponya wagonjwa, kuwaokoa waliopotea, na kufanya *lolote* ambalo amesema liwe. "Yeye anaweza katika mawe haya," Yohana kasema, "kumwinulia Ibrahimu watoto."

119 Naye mjumbe wa kweli kutoka kwa Mungu huamini hilo na kushikilia hilo. *Yehova-yire*, "Mungu atajipatia."

Mungu anaposema jambo lolote, "Litatukiaje, Ndugu Branham?"

Sijui, si kazi yangu kujua, Mungu atalijalia. Mungu atajipatia Mwenyewe.

120 "Sasa, angalieni hapa, Ndugu Branham, daktari alisema nilikuwa na kansa, naye akaniambia ya kwamba nilikuwa ninaenda kufa, nina siku thelathini bado za kuishi, alisema nilikuwa ninaenda kufa. Sasa, jinsi gani kamwe *Kitu* nisichoweza kuona, kugusa, kuhisi, kunusa, kuonja, ama chochote kile, *Kitu* kama hicho kamwe kitaondoaje kansa hii kutoka kwangu? Ni kitu gani kitakachoshuka hapa na kuiondoa kansa hiyo kihalisi?"

Sijui, lakini Mungu aliahidi jambo hilo, na Mungu anaweza kutoa kitu cha kufanya hivyo.

121 Mungu atatoa, Yeye ni Yehova-Yire, Yeye ni Yehova-Yire sasa hivi kama alivyokuwa wakati huo. Yeye angali ni Yehova-Yire, Bwana atajipatia Mwenyewe njia ya kulitimiza Neno Lake. Amina. Kama Wapentekoste hawatalipokea, Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto; kama Wabaptisti hawataki, basi Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.

122 Ninakumbuka wakati Malaika wa Bwana alipokutana nami huko nje usiku ule, wakati aliposhuka mtoni pale na kusema maneno hayo mbele ya watu kama elfu kumi. Akaniambia, kasema . . . Umeusikia ujumbe, aliyosema yako kwenye kitabu. Angalieni jinsi ulivyotimia hasa, kikamilifu neno kwa neno, hakika, maneno yale yale aliyosema yapata miaka thelathini na

mmoja iliyopita, akaniambia mahali ningeenda, na la kufanya, na kile ingesababisha. Mungu alisema . . .

123 Ndipo nikamwendea mchungaji wangu wa Kibaptisti na kumwambia, akasema, "Huku ukiwa na elimu ya darasa la saba? Ati utahubiri Injili kote ulimwenguni, na kufanya miujiza na ishara?"

Nikasema, "Hivyo ndivyo alivyosema."

Kasema, "Billy, ulikula chakula gani cha jioni usiku huo?"

Nikasema, "Afadhali niirudishe kadi yangu ya ushirika sasa hivi, kwa sababu Nuru na giza haviwezi kushirikiana." Hiyo ni kweli kabisa.

Akasema, "Unafikiri ni nani angekuamini?"

124 Nikasema, "Kama Mungu ananituma, Mungu atakuwa na mtu fulani huko nje wa kuupokea Ujumbe, kwa sababu Mungu hafanyi hivyo bure."

125 Ndipo nilipowaona Wapentekoste nilipiga kura yangu pamoja nao, kweli kabisa, kwa sababu waliliamini, walikuwa wakilitafuta, waliamini kwamba ni kweli. "Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Naam, bwana.

126 Kwa hiyo kama Mungu alituma Ujumbe, Mungu aliuahidi katika Biblia, Mungu alisema angefanya hivyo, Yeye aliahidi angefanya hivyo, Yeye alisema, "Ishara hizi . . . " Alisema ishara zizi hizi na maajabu yangetukia kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma.

"Itatukiaje?"

Sijui, siwezi kuwaambia. Yeye aliahidi angetuma mambo haya yote, nayo haya hapa yanatendeka.

"Inafanyaje kazi, Ndugu Branham?"

Laiti ningalijua, sijui, bali Mungu aliahidi jambo hilo, naye Mungu ni Yehova-Yire, Yeye anaweza kuandaa njia ya kulifanya. Amina.

127 Yeye angeweza kutoa katika madhehebu, kutoka kwenye dhehebu fulani, ama—ama chochote anachotaka kufanya, anaweza kufanya atakalo kwa sababu Yeye ni Mungu, Yehova Mungu. "Yeye anaweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Yeye ni Yehova-Yire.

128 Nawatakeni myaweke hayo maneno niani mwenu sasa, nimewaweka kwa dakika ishirini zaidi, bali nataka myaweke mambo hayo niani mwenu.

"Mungu ataniponyaje?" "Mama yangu, Ndugu Branham, ni mgonjwa sana." "Mtoto wangu mchanga ni mgonjwa sana, *hili* ni *lile*."

"Unaweza kuwasaidia?"

"La, hakuna kitu ninachoweza kufanya."

"Vema, ulisemaje . . . ?"

"Vema, Mungu anaweza kufanya."

"Vema, Yeye atafanyaje jambo hili? Mtoto huyu alizaliwa hivi."

129 Nimeona maelfu mara maelfu waliozaliwa wakiteseka, kichwa kilichojawa maji, waliokunjamana, na kadhalika, ambao ni wa kawaida kabisa na ni wazima kabisa leo hii.

"Alifanyaje jambo hilo?"

130 Sijui. Jambo pekee nijualo, Yeye ni Yehova-Yire, Bwana ametoa Dhabihu, Bwana ametoa Mwa—Mwana-kondoo. Kumbukeni, haikuwa ni kondoo jike, ilikuwa ni kondoo dume; Yesu alikuwa Mwanamume, Mwanamume alikuwa Mungu, Mwanamume, Mungu aliishi ndani yake. Naye alikuwa ndiye Kondoo mume wa sadaka, Naye tayari ametoa, haitubidi kumngojea Yeye aje, ama *kitu kingine* dhabihu ipate kutolewa, tayari imetolewa. Na jambo pekee tunalopaswa kufanya ni—ni kuweka matumaini yetu na imani katika Dhabihu ya Mungu ambayo tayari imetolewa.

"Unajuaje imetolewa?"

Vema, Huyu hapa, moja kwa moja miongoni mwetu, akifanya mambo yale yale aliyofanya duniani. Amina. Mnampenda?

Na tuinamishe vichwa vyetu.

131 Bwana Yesu, jalia lisipite juu ya kichwa cha watu, Bwana, jalia limiminike moja kwa moja ndani ya kila moyo. Jalia tuone Roho Wako mkuu akitenda kazi katika kusanyiko hili usiku wa leo, na kuwaona watoto wa Mungu waliolala hapa wakiwa wagonjwa, huku wamepita uwezo wa madaktari . . . Tunakushukuru kwa ajili ya madaktari wetu, na maarifa yote waliyo nayo, lakini, Mungu, zaidi ya yote tunakushukuru kwa ajili ya Yesu Kristo.

132 Nami naomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utamruhusu kila mmoja leo, wanapoenda nyumbani, na kusoma, na kuwaita majirani, na kuwaleta watu hao hapa nje saa kumi na mbili, usiku wa leo. Yehova Mungu na awape njia ya kuja; Yeye angali ni Yehova-Yire.

"Ninawezaje kuwafanya waje?"

Bwana, kama tungali tutafanya sehemu yetu, Wewe unaweza kutoa sehemu Yako. Na iwe hivyo Baba.

133 Waponye wagonjwa, waokoe waliopotea, jipatie Mwenyewe utukufu, kwa kuwa yote ni kwa ajili ya utukufu Wako, Bwana. Si kitu kwetu, sisi ni ninii tu, sisi, ni huruma zetu, moyo wetu, tunaona ya kwamba ingewasaidia watu, ni kitu cha kulisaidia kanisa. Kwa nini tuwe hapa? Ingekuwa bora zaidi kwangu kuwa nyumbani asubuhi ya leo maskanini mwangu, na pamoja na mke

wangu na watoto, kuliko wao kunipigia simu wakilia, nikiwa mpweke?

134 Na, Ee Mungu, hivi nimetumia miaka thelathini na mmoja ya maisha yangu nje hudumani hapa, jinsi ingekuwa rahisi kwangu kwenda nyumbani, lakini, Mungu, *Kitu fulani* ndani ya moyo wangu kinasema, "Kaa huko kwenye Pwani ya Magharibi kuliko na dhambi tele. Kaa huko ambako ukuta wa mashariki na magharibi zinakutana, na kama upepo ukipitia mbio kote, na kupulizia uchafu kwenye Pwani hii ya Magharibi huku, ambako dini potovu, na kadhalika, ambazo hazijulikani mahali pengine popote nchini."

135 Mungu, kwa nini tusimame hapa? Kwa sababu ni agizo Lako. Tutazivunjaje hizi kuta? Sijui, Bwana, lakini Wewe ni Yehova-Yire ambaye anaweza kujipatia Mwenyewe njia. Tutasimama kwenye. . .kwa sababu mioyoni mwetu, tunajisikia ya kwamba tunaweza kulisaidia Kanisa Lako dogo la thamani, ambalo linajitahidi hapa kwenye pwani hii miongoni mwa madoido haya yote ya Hollywood, na upuuzi huu mwingine wote.

136 Mungu, kwa namna fulani, Wewe utawaita Wateule Wako. "Wale aliotangulia kuwajua, aliwaita; wale aliowaita, aliwahesabia haki; wale aliowahesabia haki, amewatukuza." Bwana, wako hapa mahali fulani, sema nao Bwana, tunapofanya kazi na kujitolea kwa upendo ku—kulitoa Kanisa Lako kutoka kwenye machafuko. Tujalie, Baba.

137 Tunawakabidhi Kwako, na kujikabidhi wenyewe Kwako, kwamba Wewe utafanya kazi kupitia kwetu ili tuweze kuwa mfano katika ujirani huu, makanisa mengine, na watu wengine hapa wataona maisha ya Wapentekoste, wataona kwamba wao ni watu tofauti, wao ni watu wa kipekee, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu. Mungu, tujalie. Kanisa Lako na litakaswe na kuwekwa kando, lililoitwa litoke, likatengwa na ulimwengu wote. Tujalie, Bwana, watu wa kipekee, ishara na maajabu yakitenda kazi kupitia kwao, mikutano mikuu, yenye utukufu, na nguvu, ndipo watajua ya kwamba kuna kitu tofauti.

138 Ulisema, "Ninyi ni chumvi ya dunia, lakini chumvi ikipoteza ladha yake, itafanywa ya kukanyangwa." Watu watasema tu, "Vema, mnanena juu ya Kuja kwa Kristo, basi angalieni yale mnayofanya. nanyi mnasema ati ninyi ni tofauti, hatuoni tofauti yoyote kwenu."

139 Ee Mungu, funga kinywa cha makafiri. Tujalie Bwana. Lifanye Kanisa Lako kuwa tofauti sana, lililokolea chumvi sana hata watu watasema, "Kama kuliwahi kuwa na kundi la Wakristo, hao *hapo*. Wao ni tofauti kabisa." Tujalie, Bwana.

140 Nawe ulisema, "Nikiinuliwa juu, nitawavuta watu wote Kwangu." Na tujalie maishani mwetu, na shuhuda zetu, tukuinue, ili ulimwengu upate kumwona Mwokozi kwa ajili ya ulimwengu. Tujalie, Yehova-Yire mkuu, kwa kuwa tunaomba,

katika Jina la Dhabihu Yako uliyotoa, Mwanao Mwenyewe, Yesu Kristo. Amina.

> Nampenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

141 Loo, hilo si linakufanyia jambo fulani? [Ndugu Branham anavumisha *Nampenda*—Mh.] Tungefanya nini bila Yeye? Vipi kama hakukuwako na Yesu? Ningefanya nini leo? Ningeenda wapi?

142 Wewe, Ee Bwana, unayo Maneno ya Uzima wa Milele, ninakugeukia Wewe. Acha ulimwengu ufanye watakalo, bali Wewe unao Uzima wa Milele, jalia nishikamane Nawe, Baba yangu.

143 Vipi kama hakukuwa na Baba, hakukuwa na Yesu, hakuna upendo tu, hakuna matumaini, ningefanya nini? Tungefanya nini? Loo, siwezi, kama ningalikuwa na ndimi elfu kumi, nisingeweza kuonyesha ibada kumwabudu kutoka moyoni mwangu. Jambo pekee ninaloweza kufanya ni kusema:

> Nampenda, na . . .

Mkumbatie, ukumbatie Utu Wake, kwa imani moyoni mwako.

> . . . Yeye kwanza . . . (Yehova-Yire mkuu!)
> Na kununua . . . wokovu
> Mtini Kalvari.

144 Loo, si ingekuwa ni ajabu kama Roho akishikilia, sasa hivi tu, jinsi anavyotaka, viwete, wanaoteseka, wagonjwa, wakiinuka tu? Loo, ingeuwasha moto ukanda huu wa pwani! Magazeti yangekuwa yakizungumza, kama kila moyo ungeweza kujitolea, "Maajabu Ya Assemblies of God Katika Long Beach, Jumapili Moja Adhuhuri." Kama kuna siku zijazo, wangesema, "Wote walikuwa katika moyo mmoja, na kwa ghafla *Kitu fulani* kikaingia kanisani."

Loo, jamani, jinsi ninavyojisikia! Ninaangalia chini . . . Loo! Hebu mimi . . . Samahani, tafadhali, kwa kuchukua wakati.

145 Nilikuwa nikijaribu kumtafuta Oral Roberts asubuhi ya leo kwenye televisheni iliyomo chumbani mwangu, hatimaye nikaipata. Nikaendelea, nilikuwa nikioga, pia nilikuwa nikinyoa, nami nikaangalia, nikarudi nyuma kuona kilichokuwa kinaendelea, na, mbona, kitu kiovu kuliko vyote! Wakijaribu kutangaza sketi za wanawake, walisema zilionyesha kila msogeo wa mwili wao. Jinsi gani? Mungu akimfanya mwanamke kitu cha juu sana kama alivyo, naye angedhalilisha akili yake, huku Mungu aliweka juu yake ngozi ya kondoo apate kumficha, naye angetaka nguo iliyofumwa ipate kuonyesha kila umbo la mwili wake!

146 Enyi Wakristo, hivi hamwezi kuhisi uovu huo? Kama huwezi, kuna kasoro. Inanihuzunisha, nikageuka, nikawaza, "Ee Mungu, sijui kama dada zangu wa Kipentekoste wangeninii . . . Tafadhali Mungu, usiache hilo litendeke, tafadhali, uturehemu, Mungu, usifanye hivyo, usiwaache wachukuliwe na upuuzi huo."

147 Nikatoka mtaani, nikawazia ningepata kiamshakinywa kidogo, akaja mtu na mkewe, wakienda kanisani, na mwanamke huyo akipulizia moshi wa sigara kutoka pande zote mbili, kama injini ya mvuke, ama kitu fulani; huyu hapa nyanya anashuka mtaani, amevaa viatu virefu, akayumba upande *huu*, huko nyuma kabisa upande *huo*, na huko nje kabisa upande *huu*. Sifanyi mzaha, ninajaribu tu kuwaambia.

148 Basi nafsi yangu ikahuzunika sana, nikawazia, "Mungu, mimi huyu hapa nje kama mhudumu wa haki, nami ninaweza kulikemea, nalo linawafanya wanichukie. Nifanye nini, Bwana? Nifanye nini? Ni watu Wako!"

Ndipo kitu Fulani kikaniambia, "Je, ungetamani sifa za wanadamu kuliko sifa za Mungu?"

149 Nikasema, "Bwana, nipe ujasiri. Hebu watu waone ya kwamba ni upendo, si nipate kuwa tofauti, ni upendo. Ninajaribu kunena wokovu, mnaona, katika Kanisa langu dogo ambalo Yesu alilifia."

150 Basi nikaketi chini pembeni, nikaketi pale, nami nikaangalia, na hawa hapa wasichana wawili au watatu wanakuja, wakivuka barabara, huyu hapa mvulana mmoja anakuja pamoja na mmoja wao, hiyo mitindo ya Riki ya kukata nywele, mwajua, huku wakienda zao, nikawaza, "Ee Mungu!" wametoka kanisani, sigara mkononi. Nikaangalia, wakishuka kwenye mtaa mwingine, na hili hapa genge zima linakuja, mmoja wao akifanya mzaha wa kuchekesha sana, utovu wa uadilifu.

151 Nikaanza kutembea mtaani, nikawaza, "Mungu, haya siyo Makazi yangu. Kwa nini usiniache tu—nipoteze tu nguvu za uvutano, nitoke hapa wakati fulani? Nijalie niende, Bwana." Nikawaza, "Loo, siwezi kusema hivyo. Ee Mungu, ni nani atakayepaza sauti? Tutafanya nini? Tutafanya nini?" Ndipo nikahisi tu kana kwamba Kitu fulani kilikuwa kikishuka moyoni mwangu, ndani kabisa, nikawazia, "Unamaanisha ya kwamba watoto Wako, binti Zako, wana Wako, wametekwa na jambo hili, Mungu? Je, wametekwa na jambo hili?"

152 Ndipo ikaonekana kana kwamba ningeweza tu kuona, halikuwa ni ono, niani mwangu tu, ningeweza kumwona Yesu akiangalia juu ya Yerusalemu, machozi yakitiririka mashavuni Mwake, na kusema, "Yerusalemu, Yerusalemu, ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya, kama kuku awakusanyavyo vifaranga vyake, jinsi ningetaka kuwakusanya, wala hamkutaka!"

153 Nami ningeweza kumhisi Roho moyoni mwangu akilia, "Loo, Pentekoste, Pentekoste, ni mara ngapi ningewachukua ninyi chini ya mbawa Zangu, lakini hamkutaka!"

154 Kwa hiyo nadhani saa ya utengano inakaribia. Loo, enyi Wakristo, mlioitwa na Mungu, msiache hicho kiwe ndicho kikomo che—chenu. Angalieni juu, angalieni juu, jikatilieni mbali na kila mstari, achaneni na mambo ya ulimwengu, msiishikilie dunia, abirini kwenye kilindi, mwingie kilindini. Fanyeni hivyo, sivyo?

155 Baba, Mungu, ninaomba ya kwamba utawafanya watu wajue ninalomaanisha, lijalie. Na jalia waelewe ya kwamba sababu pekee ambayo maskini, mtu asiye na elimu angeruhusiwa kufanya mambo haya ni kuwafanya watambue, Bwana, saa tunayoishi, hukumu. Wanasoma magazeti, wanayasikia kwenye redio, kupitia televisheni, sayansi inasema ni dakika tatu sasa ifike usiku wa manane, na chini. Ni kitu gani kingeweza kutokea wakati wowote? Ile saa iko tayari kupiga, ulimwengu uko kwenye mwisho.

156 Tunaona ya kwamba kila taifa dogo lina mabomu yao ya atomiki na haidrojeni, baadhi yayo yangelipua shimo ardhini lenye kina cha futi mia moja na sabini na tano kwa maili mia moja mraba. Ee Mungu, ingefanya nini kama mojawapo—mojawapo ikiachiliwa na kuingia kwenye skrini hizo za rada? Kila taifa litaanza kuyarusha, ndipo mwisho umewadia. Sijui, huenda ikawa ni leo, Baba, sijui, bali nitaishi kana kwamba ilikuwa ni leo. Tujalie, Bwana, Wewe nisaidie kufanya hivyo, si mimi tu, bali wasaidie watu hawa kufanya hivyo, Bwana, jalia tujiweke tayari.

157 Yesu alitwambia, "Mambo haya yatakapoanza kutokea, inueni kichwa, ukombozi unakaribia." Nasi tunaiangalia Israeli, kalenda ya Mungu, wameketi huko katika nchi ya uenyeji wao, wakingojea kumwona Masihi, Israeli walirudi, wakati Yusufu atakapojitambulisha. Kutakuwako na kilio, kila familia ikijitenga, ikilia. Lakini kabla ya hilo kuja, alifanya nini? Alimpeleka mkewe katika ikulu.

158 Ee Mungu, tujalie, tujalie, Bwana, kwamba kanisa litaona jambo hilo upesi. Tunajua ya kwamba wote hawatafanya hivyo, kwa sababu Wewe ulisema ya kwamba watakuwa vuguvugu, ingekubidi kuwatapika kutoka kinywani Mwako, lakini maskini masalia wangeingizwa ndani. Mungu, jalia kwamba kila mtu hapa leo ataitwa hao maskini masalia, jalia, jalia wapate thawabu ndogo ya masalia.

159 Libariki kanisa hili, Mungu. Kanisa hili dogo lililoko pembeni hapa, hapana shaka lilijengwa, Bwana, chini ya upinzani mkubwa. Tunajua ya kwamba watu wengi ambao wamekuwa wafuasi wa dhehebu ambalo kanisa hili linawakilisha, Assemblies of God, ninaweza tu kusikia shuhuda

hizo kutoka kwa hao wazee wakati wao, hao wanawake wazee wangepaza sauti, nakumbuka juu ya mtu aliyerusha bastola ya .45 ya Colt humu chumbani, na kumpiga mwanamke huyu moja kwa moja kwenye aproni, nazo hizo risasi zikaanguka sakafuni, maskini mama mcha Mungu wa Assembly of God. Angesema nini kama angeweza kuamka asubuhi ya leo na kuwaona binti zake? Ee Baba Mungu, uturehemu, utufanyie jambo fulani upesi, Bwana. Tujalie.

160 Mungu, siwezi kujizuia kusema mambo haya, kuna Roho ndani yangu anayelia, analia, yakitiririka tu na kulia. Ninaomba rehema, Bwana. Watu hawa hunipa sadaka ya upendo, ambayo ni sehemu ya riziki zao, Bwana, kuwapatia watoto wangu riziki, nisingewadhuru, Wewe unajua nisingewadhuru, Bwana, na—nawapenda sana. Lakini Mungu, ni—nifanye nini ila tu kumfuata Roho Wako? Ninaomba ya kwamba utayaweka wazi yaliyosalia, Bwana. Jalia, kwamba watafahamu, na, sote pamoja, sote tutaokolewa katika kule Kuja kukuu kwa Bwana.

161 Ninawakabidhi mikononi Mwako, na kujikabidhi mwenyewe, Bwana. Niongoze kwao, na wao kwangu. Tujalie, Baba, kwamba tuweze kuwa kanisa la Mungu aliye hai, lilliounganishwa pamoja kwa upendo, na vifungo vya upendo, kwa Roho Mtakatifu. Hatuwezi kufanya hivi sisi wenyewe, inahitaji Roho kulifanya, kwa hiyo, Baba, tunajikabidhi mikononi Mwako, katika Jina la Mwanao, Yesu Kristo, Mwokozi wetu. Amina.

162 Mpaka nitakapowaona usiku wa leo saa kumi na mbili. Leo, Gene, Ndugu Borders, Billy, ama baadhi yao, watakuwa hapa kusambaza kadi za maombi, labda, Billy, hiyo ni kazi yake. Atakuja hapa usiku wa leo, azichanganye hizo kadi, na kumpa kadi mtu yeyote anayezitaka. Ndipo tutaita kutoka mahali fulani mle usiku kucha.

163 Sasa, huenda tukawa na mmoja zaidi, Jumapili juma lijalo. Sasa, waingizeni watu wenu humu ndani. Hatujui kama tutalifanya au la, hivyo ndivyo Roho Mtakatifu atakavyoongoza, chochote afanyacho. Lakini sasa, wakati mwingine anajitokeza mikutanoni, anakuwa mwingi sana siwezi kumkomesha, anaendelea tu, kwa vyovyote vile. Nami si—sijui litakalotukia, najua ninampenda tu Bwana, ninawapenda.

Mnasema, “Ati unatupenda, na kutuzungumzia namna hiyo?”

164 Hiyo ndiyo sababu, ninawapenda, hiyo inaonyesha ninawapenda. Sitaki mpotee, ninataka kuishi Milele pamoja nawe, ndugu yangu, dada yangu. Sijaribu kuwafanya mnikasirikie, ninawapenda sana. Hivi baba halisi angemwona mtoto wake ameketi barabarani, na kusema, “Kitoto changu kichanga, afadhali wewe. . .?” Loo, la, angemrudi, angefanya yote awezayo kumzuia asiuawe.

165 Nitakaposimama kule Siku hiyo, na kumtazama Yeye, vipi kama Roho Mtakatifu angesema, “Nilikutia mafuta, na kukutuma, nawe ukasitasita”?

Nawe ungenipungia mikono yako, na kusema, “Ndugu Branham, laiti ungaliniambia!”

166 Huh-um. Haitakuwa hivyo kwangu, nitakuwa mwaminifu kwenu, nitakuwa mkweli kwenu, maana kweli nawapenda, na Mungu ananishuhudia ya kwamba hiyo ni kweli.

Mpaka nitakapowaona usiku wa leo, mchungaji.

Mungu akubariki, Ndugu Buntain.

61-0212M Yehova-Yire
First Assembly Of God Of Long Beach
Long Beach, California Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org